



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA**  
**SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA**  
**CHUNYA**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na CDC/NM/05

Tarehe: 09/08/2022

**TANGAZO**

**MWALIKO WA ZABUNI**

**UFUNDI UJENZI WA JENGO LA IDARA YA WAGONJWA WA NJE(OPD) NA**  
**WODI MAALUM (GRADE A") HOSPITALI YA WILAYA NA NYUMBA YA**  
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YACHUNYA.**  
**ZAB; NA. LGA/075/2022/2023/FA/ 02**

1. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anawatangazia mafundi ujenzi (Loal Fundi) Uashi, na wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ufundi wa kujenga majengo/nyumba za serikali kuomba kazi za ufundi ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya na ujenzi nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chunya. Zabuni hii imerudiwa kutokana na ongezeko la nyaraka pamoja na sifa hitajika kwa waombaji.
2. Kazi imegawanyika katika makundi (LOTs) na kila kazi inajitegemea. Mwombaji unaruhusiwa kuomba kazi zaidi ya moja kwa kutegemea uwezo wako. Makundi ya kazi ya ufundi yamegawanyika kama ifuatavyo

ZABUNI NA.	MAELEZO YA KAZI
LGA/075/2022/2023/FA/02	LOT 1- Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) Hospitali ya Wilaya ya Chunya.  LOT 2- Ujenzi wa jengo la wodi maalumu (GRADE A) Hospitali ya Wilaya ya Chunya.  LOT 3- Ujenzi nyumba ya mkulugenzi wa halmashauri na

	jengo la wageni ndani ya makazi ya mkulugenzi Wilaya ya Chunya.
--	---

3. Mwombaji awe amepitia mafunzo ya ufundi kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali kama vile VETA. Sifa za mafundi wanaohitajika

NA	AINA ZA MAFUNDI WANAOHITAJIKA	SIFA ZINAZOTAKIWA
A	Fundi uashi	<ul style="list-style-type: none"> <li>i. Ajue kusoma ramani na kutafsili ramani</li> <li>ii. Ajue kujenga kwa mawe na matofali</li> <li>iii. Ajue kupiga lipu kuta za mawe na tofali</li> <li>iv. Ajue kuweka sakafu vizuri na iliyonyooka</li> <li>v. Ajue kuweka marumaru (tiles)</li> <li>vi. Ajue kuseti masinki ya vyoo</li> <li>vii. Ajue kumaliza lipu (skimming)</li> <li>viii. Ajue kutumia zege</li> <li>ix. Aijue michanganyo ya mota</li> <li>x. Ajue kuchanganya saruji (cement) na mchanga</li> <li>xi. Ajue kuweka tarazo</li> <li>xii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuonyesha sehemu alizofanya</li> <li>xiii. Ajue vifaa vya fundi uashi</li> <li>xiv. Ajue kuchanganya rangi</li> <li>xv. Ajue matumizi ya rangi</li> <li>xvi. Ajue aina za rangi</li> <li>xvii. Ajue vifaa vya fundi rangi</li> <li>xviii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizopaka rangi</li> <li>xix. Awe na uwezo wa kujenga hidden roof.</li> </ul>